



INTERNATIONAL
TRANSPORT
WORKERS'
FEDERATION

VIWANGO

SALAMA

HUOKOA MAISHA

JIUNGE NA VITA VYA KUPIGANIA AJIRA NZURI NA BARABARA SALAMA

MALIPO YA JUU HUPUNGUZA AJALI ZA BARABARANI

Malipo ya haki katika usafiri barabarani:

- husababisha upungufu wa ajali barabarani
- huimarisha usalama barabarani
- yanawezaifanya sekta yetu endelevu zaidi

**UTAFITI UNAONYESHA KWAMBA NYONGEZA YA
MALIPO YA 10% YAWEZAPUNGUZA AJALI HADI 30%**

VIWANGO SALAMA NDIYO JAWABU

Sisi sote hunua kuenda nyumbani baada ya siku mzima kazini.

Kama wafanyakazi wa usafiri barabarani, tunakabiliwa na shinikizo kubwa la kuendesha gari kwa saa nyangi, kufanya kazi tukiwa tumechoka, kuendesha kwa kasi, na kupakia magari yetu kupita kiasi. Hailalishi ni kampuni gani unaifanyia kazi, au weve ni mfanyakazi au deraeve mmiliki. Shinikizo tunalopata huanzia juu kutokana na mazoea ya bei ya chini ya kutoa zabuni na madai yasiyo na maana yanayotolewa na makampuni makubwa ambayo yana kandarasi ya huduma za usafiri barabarani ndiposa usafirishie bidhaa zao. Shinikizo za kiuchumi hutirika kutoka juu kwa kampuni hizi kubwa za wateja hadi kampuni za usafirishaji na hadi kwetu, na kufanya kuwa ngumu kuepukana na mazoea hatari barabarani, na kuhatarisha maisha ya watumiaji wote wa barabara.

Viwango Salama vinaweza kukomesha taratibu hizi za biasara zisizo endelevu na kuhakikisha malipo na masharti ya haki kwa madereva na barabara salama kwa kila mtu.

VIWANGO SALAMA VINA MAANISHA NINI KWANGU?

Viwango Salama vinaweza hakikishwa kupitia makubaliano ya muungano na waendeshaji usafiri na wateja wao, au katika mifumo ya udhibiti wa kisheria ambayo:

- inaweka viwango vya malipo na masharti ambayo ni ya haki na sawa kwa madereva wote
- inawayibisha wahusika wote wa ugavi, ikijumuisha makampuni yaliyo juu
- inashirikisha vyama vya wafanyakazi katika mchakato wa kuweka, kufuatilia na kutekeleza viwango

Kwa dereva, 'Viwango Salama' yamaanisha kwamba unalipwa kwa haki kwa muda wako wote wa kazi na kupata pesa za kutosha kuendesha gari kwa usalama na kukimu mahitaji ya familia yako.

Ikiwa unamiliki gari lako, ni lazima Viwango Salama vihesabiwe ili kuhakikisha kwamba

unaweza kulipia gharama za kulinunua, kulitunza na kuliendesha.

Kwa waendeshaji usafiri, viwango salama vinamaanisha bei za kandarasi zinazowezesha kuhakikisha viwango vya haki na salama kwa madereva wote. Yani, bei nzuri inalipwa kwa usafiri.

IMETHIBITISHWA KIMATAIFA

Mifumo ya Viwango Salama imeboresha maisha ya wafanyakazi wa usafiri wa barabarani na familia zao, imeimarisha usalama barabarani, na kufanya usafiri wa barabarani kuwa endelevu zaidi katika mataifa ulimwenguni kote zikiwemo Canada, Brazili, Australia na Korea Kusini.

Viwango Salama katika jimbo la New South Wales nchini Australia vimeokoa zaidi ya maisha 205 ambayo yanagepotezwa katika ajali za lori.

Baada ya miaka 2 ya kutekeleza Viwango Salama nchini Korea Kusini, uzoefu wa madereva kusinzia wanapoendesha ulipungua kwa zaidi ya 60%.

JIUNGE NA KAMPENI YA KIMATAIFA YA VIWANGO SALAMA

Kwa pamoa, tupiganie Viwango Salama vya haki, barabara salama na sekta endelevu ya usafiri barabarani.

Ulimwenguni kote, madereva wanatoa mwito:

- Serikali ilinde Viwango Salama.
- Bei nzuri ya usafiri ambayo inahakikisha madereva wanaweza kulipwa kwa haki
- Mikataba ilioandikwa kwa uwazi kwa wafanyakazi wote, ili Viwango Salama viweze kufuatiliwa na kutekelezwa
- Adhabu kwa kampuni zinazokiwa Viwango Salama, zikiwemo kampuni zile za juu
- Haki ya kuwakilishwa na chama cha wafanyakazi na sauti yako kusikilizwa
- Serikali na Kampuni kuheshimu viwango vya kimataifa vya kazi vinavyohusiana na Viwango Salama.



JUZWA MENGI ZAIDI KWA KUWASILIANA NA MUUNGANO WAKO